


Kutokana na Kisa Halisi cha Maisha


# Mradi wa Kufuga Ng'ombe

Mwandishi: Olivia Wood
Tafsiri: Mourice Wabwire
Mchoraji: Ching Yun Wu

ASHOKA
Worldreader

“Mradi wa Kufuga Ng’ombe,” ni hadithi ambayo imechochewa na kisa halisi cha msichana aliyewaenzi sana wanyama na kutumia upendo huo kubadilisha maisha ya mamia ya wakulima na ng’ombe katika jamii yake.


Kitabu hiki cha picha cha watoto ni tukio la ushirikiano baina ya Ashoka na shirika la kibinafsi la Worldreader. Kimenuia kuwahimiza watoto wote kuwa wanamageuzi na watu wazima kuwaunga mkono katika safari hiyo.



Kila siku aliwatazama ng'ombe wakiwa malishoni kijijini mwao Indonesia. Walikuwa wanapendeza. Kwanza, kwa macho yao makubwa, masikio yao makubwa na marefu na kope za kuvutia.

Ara alipofika umri wa miaka kumi, aliwaomba wazazi wake iwapo wangeweza kununua ng'ombe. Mama yake alisema, "Ara ni kazi nyingi kumfuga ng'ombe." Na babake akasema, "utahitaji kuiosha na kuikama maziwa kila siku."


Ara aliahidi kuwa angezifanya kazi hizo zote. Alikuwa amejitolea na aliwaenzi ng'ombe sana.



Siku moja hewa ilikuwa na unyevu wenye joto kali. Ara alikuwa akiwatazama ng’ombe wakicheza, wazazi wake walimjia na kusema, “Iwapo tutatenda kununua ng’ombe, tunahitaji kujifunza kuhusu ng’ombe kutoka kwa wakulima.”

Shamba la kwanza walilolitembelea lilikuwa la kufana mno! Ng’ombe hapo walinukia  vizuri huku wakitafuna majani wakiwa wasafi na wenye furaha.

“Ng’ombe wetu wana furaha kwa hivyo hutoa maziwa mengi sana,” Mkulima mmoja alimwambia Ara. Alimpa baadhi ya maziwa aonje, yalikuwa matamu na mazito.



Shamba la pili lilikuwa tofauti sana, ng’ombe walikuwa na matope. Harufu iliyoje! Kulikuwa na wadudu kila mahali wakivuma machoni mwa ng’ombe.

“Hii si hali nzuri,” alifikiri Ara. “Ninataka ng’ombe hawa wawe na furaha.”

Wakati Ara aliuliza kuhusu utoaji wa maziwa wa ng’ombe hawa, wakulima walitikiza vichwa vyao. “Hatupati maziwa mengi kutoka kwa ng’ombe wetu.”



Usiku huo, Ara hakuweza kulala. Alijawa na fikra kuhusu ng’ombe wasiokuwa na furaha na wenye uchafu mwilini mwao.

“Mtu anapaswa kuwasaidia,” Alifikiria. Mwanzoni ilionekana ni vigumu. Je angewezaje kuwasaidia?

Kisha likamjia wazo: “Labda wakulima wa kwanza wanaweza kuwasiaidia wakulima wa pili.”



Asubuhi iliyofuata Ara alizungumza na mamake kuhusu wazo lake, Ara pamoja na mamake waliibuka na mpango wa kuwasaidia ng'ombe na wakulima.

Ili kuanza, walirudi kwa shamba la kwanza. Ara aliuliza iwapo wangeweza kuwasaidia wakulima wenzao kwa kuwafunza jinsi ya kuwatunza ng'ombe. Na wakakubali.

Kisha walifululiza hadi shamba la pili. "Nyinyi hamna maziwa mengi," alisema Ara, "Ila wakulima wengine wanaweza kuwafunza jinsi ya kupata maziwa mengi."




Ara aliianda mkutano wa wakulima. Siku ya mkutano, Ara alijawa na wasiwasi. “Je itakuwaje iwapo sitaweza kuwasaidia ng’ombe?” Alitafakari.

Mkutanoni, mkulima wa kwanza alisimama na kushiriki siri zake za kuwaweka ng’ombe salama.


Baada ya mkutano wakulima walimshukuru Ara. Siku ilikuwa ya kufana sana na kila mmoja alielimika sana!

.



Siku moja, miale ya jua ilikuwa utosini mwa Ara. Yeye na mamake waliamua kufunga safari ya kuwazuru ng’ombe.

Shamba zote zilikuwa safi ikilinganishwa na awali. Hukukuwa tena na wadudu na matope kwa ng’ombe, na palikuwa na hewa safi mithili ya majani mabichi. Wakulima pia walisema walikuwa wakipata maziwa mengi!




Mmoja wa wakulima alitabasamu alipomuona Ara. Uso wake ulikuwa na makunyanzi na upole. “Asante sana kwa kutusaidia kujifunza mengi,” mkulima alisema. “Tunataka sasa kukutana na wakulima wengine ili tuwadokezee siri yetu.”

Katika mkutano uliofuata kulikuwa na wakulima wengi. Wakulima wengine walikuwa wamewakaribisha rafiki na jirani zao kuhudhuria!

Baada ya mkutano, Baba yake alimkumbatia Ara. “Umeleta mabadiliko katika jamii yetu,” alisema. “Ni ya kustaajabisha yale ambayo msichana mmoja ameweza kuyafanya.”



Usiku huo, Ara alienda kulala polepole huku akifikiria kuhusu ng'ombe na watu ambao alikuwa amewasaidia. "Unaweza kuleta mabadiliko ukiwa umri wowote," alitafakari na kujivunia. Je mabadiliko yapi tutaleta tena?

**Tukio 1:** Kufikiria kama Ara

**Kundi-umri:** 3-8

**Ujuzi:** Huruma, Kufikiria kwa Kina

**Nyenzo:** Hakuna

**Mbono?** Hadithi hutuwezesha kufika kwenye ulimwengu dhahania na kukumbana na wahusika, hali na matukio ambayo hatungeweza kufikia katika ulimwengu halisi. Kupitia kwa hadithi, sisi huvalia viatu vya watu ambao wamepitia changamoto ambazo ni tofauti na zile zetu na kuwa na mtazamo mpya. Kwa mchakato huu tunafikia kuvidhamini vitu vilivyo karibu nasi.

**Vipi?** Safari ya Ara ilianzishwa na kitu cha kawaida tu; upendo kwa wanyama. Hebu tafakari hadithi ya Ara alipowaona ng'ombe wachafu na wenye huzuni.

1. Je, ungehisi vipi iwapo ungekuwa Ara?

2. Unadhani Ara anafikiria vipi?

3. Unajuaje?

4. Je, unaweza kumbuka wakati ambao ulikuwa na hisia sawa na Ara?

5. Nini kilimchochea Ara kuwasaidia ng'ombe na wakulima?

6. Je, unagefanya nini kama ungekuwa Ara?

**Tukio la 2:** Tikiti ya Uelewa

**Kundi-umri:** 3-8

**Ujuzi:** Uelewa, Akili ya Kijamii na kihemko

**Nyenzo:** Kipande cha karatasi, penseli

**Mbona?** Kunakili kazi za ziada huwasaidia vijana kushika na kukumbuka yale ambayo wamejifunza. Tikiti ya uelewa inaweza kutumika kama muktasari wa mawazo makuu ya hadithi ama tukio lako. Maswali ya kihisia huwasaidia vijana kugundua na kuwasilisha hisia zao na watu wengine.

**Vipi?** Uelewa hutusaidia kugundua kile kinachoendelea maishani mwa watu wengine na kufikiria yaliyo miyoni mwetu. Kwa kuuliza maswali, Ara aliweza kujifunza juu ya maisha ya wakulima na jinsi ya kuwasaidia. Baada ya kusoma hadithi ya Ara, chukua kipande kidogo cha karatasi na na unyakue penseli. Andika ama uchore vitu ambavyo umejifunza kutoka kwa hadithi ya Ara. kuwasiliana hisia zao na watu wengine.

Tafakari kuhusu:

1. Ni sehemu ipi ya hadithi ya Ara ilikufarahisha?

2. Katika hadithi yote ya Ara, amejifunza kujiamini na ujasiri huku akiwa mtu wa kujihatarisha ili kutoa suluhu. Je ni ujuzi upi Ara anao wenye unataka kujaribu?

3. Ni kitu kipi ambacho unaenda kukifanya kwa utofauti baada ya kujifunza kutoka kwa Ara?

Ibandike tikiti yako ya uelewa chumbani mwako. Baada ya kusoma hadithi nyingine, rejelea tukio hili. Pindi utakuwa umejifunza ujuzi na maoni mengi!

**Tukio la 3:** Kuwadhamini Wenzako

**Kundi-umri:** 3-8

**Ujuzi:** Uelewa, Ujenzi wa mahusiano

**Nyenzo:** Kipande cha karatasi na penseli

**Mbona?** Kufanya mazoezi ya kutoa shukrani ni tukio la muhimu sana ukijaribu kuelewa mitazamo mipya na kujifunza jinsi ya kushukuru michango ambayo tunayotegemea kila siku. Tukio lifuatalo ni muhimu sana katika kukuza usikivu wa vijana na kupanua uwezo wa kuelewa na kuwadhamini wale walioko karibu nao.

**Vipi?** Wazazi wa Ara walikuwa na jukumu kubwa kama wanamageuzi. Walimuunga mkono Ara kwa kumhimiza kukabiliana changamoto kwa sababu walijua kujifunza kuleta mabadiliko chanya ukiwa mdogo ingedumu milele. Ara aghalabu huwatolea shukrani kama malipo na kuwakumbusha jinsi ambavyo anadhamini muelekezo wao. Na tunapohisi kudhaminiwa tupo tayari kufanya kazi kwa bidi na kuwa na msimamo.

Andika ama uchore ujumbe wa shukrani kwa mtu ambaye anakuunga mkono. Yaweza kuwa ni dungu yako, mzazi, mwalimu ama rafiki. Baada ya kuadika, hakikisha unampa mtu huyu ili wajue jinsi ambavyo unawadhamini.

Tumia mfano ufuatao kuandika ujumbe wa shukrani:

Nina shukuru kwa (Taja kitu au mtu unayemshukuru) kwa sababu (elezea tofauti maalum ambayo kitu ama mtu huyo huleta maishani mwako.) Bila (Taja kitu ama mtu ambaye unamshukuru) (elezea jinsi ambavyo vitu vingekuwa na vitu ama watu hao).

Kwa hivyo ahsante sana kwa (elezea kile wanachokifanya na jinsi kinaathiri maisha yako) Taja angalau vitu viwili vyenye unawezakufanya ili kuwaunga mkono.

## MJUE ARA



Mradi wa kufuga ng'ombe ulikuwa ndio tu mwanzo wa maisha ya Ara ya safari ya uanamageuzi. Kama vijana, Ara alianzisha mradi wa *Aha!* Ambao ni mradi wa kijamii wenye fursa ya kutoa vifaa vya ubunifu na elimu bora nyumbani kwa watoto wasiojiweza mashambani mwa Indonesia.

Vilevile yeye pia ni kiongozi mwenza wa Vuguvugu la Wanamabadiliko na Ashoka kwa kuwezesha vijana kupata nguvu za kuwa wanamageuzi na kuleta mabadiliko chanya kwa changamoto zinazohusu jamii zao.

Vilevile yeye pia ni kiongozi mwenza wa Vuguvugu la Wanamabadiliko na Ashoka kwa kuwezesha vijana kupata nguvu za kuwa wanamageuzi na kuleta mabadiliko chanya kwa changamoto zinazohusu jamii zao.

## Kuhusu Ashoka

Ashoka anaamini kuwa uwezo wa kuzoea na kuleta mabadiliko ni muhimu sana kwa kila mmoja kustawi haraka kwa huu ulimwengu unaobadilika kila kuchao. Ashoka anaandaa jamii ya kilimwengu yenye msingi ambapo kila mmoja ni mwanamageuzi. Katika nyoyo za kila mmoja,Vuguvugu la Wanamabadiliko wana maono ya kubadilisha jinsi Watoto na vijana wanakua na kupata ujuzi wa kuleta mabadliko kwa mujibu wa wote.

**www.ashoka.org**

## Kuhusu  Worldreader

Worldreader inaamini kuwa wasomi hujenga ulimwengu bora. Tunafanya kazi na washikadau ulimwengu mzima na kuwasaidia watu pamoja na jamii zilizopo katika mazingira dhaifu kwa usomi wa kidijitali ambao husaidia kuimasirisha  kusoma na kuandika na matokeo ya kujifunza kwa Watoto.

**www.worldreader.org**

2021 Ashoka na Worldreader

Kazi hii imetolewa kibali chini ya *Creative Commons Attribution-NonCommercial 4.0 International License*.

Kwa ujumbe zaidi tafadahali wasiliana na **privacy@ashoka.org** ama **publishing@worldreader.org**